

KIBAHA MJI KIDEDEA KWA UFUNGAJI WA MAHESABU

Na Innocent Byarugaba, Kibaha

Halmashauri ya Mji Kibaha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imepata tuzo ya Ubora ya Ufungaji wa Hesabu za Mwaka za Halmashauri kwa Kuzingatia sheria za Kimataifa. Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha Bi jenifa Omolo kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilichofanyika leo kwenye Ukumbi wa Halmashauri hiyo.

“Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji Kibaha imepata Tuzo ya Ubora na kushika nafasi ya Kwanza kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 188 kwa kufuata na kuzingatia sheria na Kanuni za Kimataifa za Uaandaji na uwasilishaji wa Hesabu za Umma (PSAS)” alisema Omolo

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kibaha ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Msangani Mhe. Leonard Mlowe mbali na kuwapongeza Wahasibu wote kwa kazi nzuri waliyoifanya, alisema huu ni Mwanzo Mpya kwa Kibaha kuonesha umahili wake, kufanya mambo ya Kitaifa kwa maslahi ya Taifa na Kwamba hakuna sababu ya kutokuwa Manispaa.

Aidha, Mhe. Omary Bura, Diwani wa Kata ya Kibaha alisema huu ni ushindi wa Halmashauri nzima kwani imeonesha ni kwa namna gani watendaji wanavyoshirikiana na Wanasiasa pamoja na Wadau wa Maendeleo kuhakikisha Halmashauri inakwenda mbele.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Misugusugu Mhe. Bogasi Ramadhani alisema siku zote mtu anayefanya vema kwenye jambo zuri apongezwe na kushauri washiriki wote walioiletea Heshima Halmashauri waandaliwe mazingira wezeshi ya kuendelea kufanya vizuri na siku zijazo.

Tuzo ya Ubora na Ufungaji wa Hesabu kwa Kuzingatia Sheria na Kanuni za Kimataifa hutolewa na Bodi ya uhasibu na Ukaguzi Tanzania (NBAA) kwa Taasisi za Umma na Binafsi zilizozingatia sheria na Viwango vya Kimataifa katika kuandaa na kuwasilisha hesabu za Umma. Mwaka 2014/2015 Jumla ya Halmashauri 188 zilishindanishwa na Kibaha Mji Kuibuka ya Kwanza.